JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

IMETHIBITISHWA ISO 9001

# TAARIFA KWA UMMA

# KUTOA LESENI ZA USAFIRISHAJI NJIA YA KISESA - USAGARA KUPITIA BUZURUGA MKOANI MWANZA

***Dar es Salaam 25 Septemba, 2025***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawakaribisha wasafirishaji kufanya maombi ya leseni za usafirishaji abiria kwa njia ya **KISESA – USAGARA, Kupitia Buzuruga**, Mkoa wa Mwanza.

Utoaji wa leseni hizo utazingatia vigezo vifuatavyo:

1) Mwombaji awe ni Kampuni au Ushirika wa Wasafirishaji uliosajiliwa;
2) Awe na uthibitisho wa umiliki wa magari au Mkataba wa kukodisha magari;
3) Magari yawe na uwezo wa kubeba abiria wasiopungua 25;
4) Atumie Madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosajiliwa na LATRA;
5) Mabasi yawe na Vifaa vya Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD); na,
6) Mwombaji atumie Mtoa Huduma wa Tiketi Mtandao aliyeidhinishwa na LATRA.

Wasafirishaji waliokidhi vigezo hivyo watume maombi LATRA kupitia **rrims.latra.go.tz** mfumo wa maombi ya leseni. Aidha masharti mengine yaliyotajwa katika Kanuni za Utoaji wa Leseni kwa Magari ya Abiria, Tangazo la Serikali Na. 76 za Mwaka 2020 yatazingatiwa**.** Mamlaka itatoa kipaumbele kwa maombi yatakayowasilishwa mapema.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Thu Sep 25 18:38:41 EAT 2025

Salum PAZZY

**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**